COMPETENCE BASED CURRICULUM HOMEWORK ENGAGEMENT PROGRAM GRADE 6 2024 AUGUST KISWAHILI

1. **KISWAHILI**

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswall 1-5.

(Mwanasiasa na wananchi wamekutana katika ukumbi wa Ulimisukari ili kutathmini maendeleo *yaliyofanywa* na *ahadi* zilizotimizwa tangu mwanasiasa alipotwaa uongozi.)

Mwanasiasa: Ni matumaini yangu kuwa hamjambo. Nina furaha mpwitompwito kwa kuitikia wito huu wa kujumuika nanyi hapa. Kwanza, asanteni sana kwa kura zenu.

Mkulima: Mheshimiwa, ulituahidi mbolea ya bei nafuu. Hadi leo hatujaiona. Je, kulikoni?

Mwanasiasa: (Kwa *kiburi*) Wizara husika imegundua kuwa serikali iliyotangulia ilitumia vibaya pesa, hivyo, bado hatuna pesa. Tumieni samadi. Kunjeni mashati jamani. Endeleeni kukaza misuli!

Mzazi: Bwana Tumbo, hali ya masomo je? Uliahidi kuwa wanafunzi wetu watafanyia majaribio mwezini.

Mwanasiasa: Kuhusu hilo, naomba mnipe muda kidogo niwasafirishe wanangu warudi shuleni ng'ambo kwanza. Kuhusu majaribio mwezini, tumegundua kuwa hali ya anga huko si shwari. Watasalia chini ya miti kwa muda.

Mwalimu: Hatujaona mabadiliko katika sekta ya wafanyakazi wa umma. Ulituahidi magari kwa mkopo, sasa....

Mwanasiasa: Baiskeli hujui kuendesha, utaendeshaje gari? Mimi naona bora tufungue vyuo vya mafunzo ya udereva kwanza, ama vipi wenzangu? *(*akiangazaangaza*)*

Mjenzi: Mheshimiwa, ulituahidi vyakula bila malipo kila mwezi, kugawana mali yako na mifereji ya maziwa. Umeyafumbia macho. Mheshimiwa huoni haya?

Mwanasiasa: Jamani, naomba tuulize maswali ya kiutuuzima! Wewe uliona wapi mifereji ya aina hiyo? Hakuna cha bure! Imeandikwa **kila mbuzi atakula kulingana na urefu wa kamba yake**. Kuhusu kugawana mali yangu, nadhani hamkunisikia vizuri. Hali ni ngumu jamani. Tugawanaje mali yangu? *(*kimya) Mimi nadhani hamna mliloniitia. Tuonaneni baada ya miaka mitano. (wanafumukana kwa *huzuni)*

Kuhusu mbolea ya bei nafuu, mwanasiasa alitoa kisingizio gani?

A. Hakuwa na pesa za kuigharimia.